هَلْ يَعْتَكِفُ فِي غَيْرِ الْمَسَاجِدِ الثَّلَاثَةِ؟

JE

(MTU) ATAKAA ITIKAFU

KATIKA ISIYOKUWA MISIKITI MITATU?

1. Masjidill Haraam (Makka).
2. Masjidil Nnabawi (Madina).
3. Masjidil Aqsa (Palestina).

Mwandishi:

Abu Halima Arafat

Pongwe Tanga.

Utangulizi

Kila sifa njema anastahiki Allaah Mola Mlezi wa viumbe wote. Swala na salamu zimshukie mwisho wa Mitume, Jamaa zake na Maswahaba wake wote.

Ndugu msomaji, miongoni mwa amali nzuri mbele ya Allaah ni kueneza kile unachokijua katika elimu ijapokuwa kichache, kama Mtume ﷺ alivyosema:

«بَلِّغُوا عَنِّي وَلَوْ آيَةً»

"Fikisheni kutoka kwangu ijapokuwa Aya moja"[1].

Miongoni mwa mambo tunayojifunza na kupata faida katika hadithi hii ni uwajibu wa kunukuu ujumbe wa Mtume ﷺ na kuufikisha kwa watu ijapokuwa ni kitu kichache, kwa maana hiyo Mtume ﷺ akatumia neno (Lau - لَوْ).

Kadhaalika kuna nukuu nyingi kutoka kwa Maulamaa wetu 'Allaah awarehemu' wakiwahimiza wanafunzi kusambaza elimu, amesema Ibnul Mubaarak 'Allaah amrehemu' **"Sifahamu mimi daraja iliyo kubwa baada ya Unabii isipokuwa kueneza elimu"[2]**. Pia amesema Ibnul Jauziy 'Allaah amrehemu' **"Anaetaka amali zake zisikatike baada ya kufa kwake basi na aeneze elimu"[3]**.

Kwa kufanyia kazi hadithi hiyo nimeona niandike 'kwa taufiq ya Allaah' Makala hii kwa ajili ya kujibu swali ambalo nimeulizwa na watu mbalimbali waliosoma Makala yetu iliyotangulia 'DARASA ZA MWEZI WA RAMADHANI', kwamba: **"Je itafaa kukaa Itikafu katika isiyokuwa misikiti mitatu?"**, kwa sababu nilipoelezea mambo ya Itikafu sikuitaja hadithi hiyo ya Hudhaifa 'Allaah amridhie'.

Nikaona katika kujibu swali hilo niandike Makala maalumu kuhusu hadithi hiyo pamoja na kufuatishia maelezo ya Maulamaa wetu kwa kadri ya mahitajio.

Yaliyomo katika Makala hii:

1. Tafauti za Maulamaa kuhusu mahali pa kukaa Itikafu.
2. Dalili zilizokuja kuelezea Itikafu.
3. Itikafu inakaliwa katika msikiti unaoswaliwa swala za jamaa.
4. Je inafaa kukaa Itikafu katika isiyokuwa misikiti mitatu?

Abu Halima Arafat.

1- Bukhari (3461).
2- Tahdhiibul Kamaal (Jz. 16, Uk. 20).
3- At-Tadhkira (Uk. 55).

1. TAFAUTI ZA MAULAMAA KUHUSU MAHALI PA KUKAA ITIKAFU

Wametafautiana Salaf (wema waliotangulia) katika kauli saba ambazo amezitaja Ibn Hajar[4] (Allaah amrehemu) kuhusiana ni mahali gani pa kukaa Itikafu?

Kauli ya kwanza: Inafaa kukaa Itikafu mahali popote, hii ni kauli ya Muhammad Bin Lubaaba Al-Maalikiy (Allaah amrehemu). Na kauli hii ni yenye kukataliwa kwa itifaki ya Maulamaa ambayo ameitaja Imam Qurtubi katika tafsiri yake:

"أَجْمَعَ الْعُلَمَاءُ عَلَى أَنَّ الِاعْتِكَافَ لَا يَكُونُ إِلَّا فِي الْمَسْجِدِ"

"Wamekubaliana Maulamaa juu ya kwamba Itikafu haiwi isipokuwa msikitini"[5].

Kauli ya pili: Inafaa kukaa Itikafu msikti wowote ule hata kama hauswaliwi (umehamwa), haya ni madhehebu ya Imam Malik, Shaafi' na Daud Ad-Dwhaahiri (Allaah awarehemu), na ushahidi wao ni Aya ya Allaah:

﴿ وَلَا تُبَٰشِرُوهُنَّ وَأَنتُمْ عَٰكِفُونَ فِي ٱلْمَسَٰجِدِ ﴾

"Wala amsichanganyike nao (kwa jimai) na hali mnakaa Itikafu misikitini"[6].

Kauli ya Tatu: Itikafu inakaliwa katika msikiti ambao unaswaliwa swala ya Ijumaa[7], hii ni kauli ya Imam Zzuhri na ni miongoni mwa riwaya kutoka kwa Imam Malik (Allaah awarehemu), na dalili yao ni hadithi ya Aisha (Allaah amridhie):

"السُّنَّةُ عَلَى الْمُعْتَكِفِ أَن لَّا يَعُوْدَ مَرِيْضًا... وَلَا اعْتِكَافَ إِلَّا فِيْ مَسْجِدٍ جَامِعٍ"

"Sunna kwa mwenye kukaa Itikafu ni kwamba asimtembelee mgonjwa... wala hapana Itikafu isipokuwa katika msikiti wenye kuswaliwa 'swala ya' Ijumaa"[8].

Kauli ya Nne: Itikafu inakaliwa katika msikiti wenye kuswaliwa swala ya jamaa, haya ni madhehebu ya Abu Hanifa, Ahmad, Is-haaq na baadhi ya Salaf (Allaah awarehemu), dalili yao ni hadithi ya Aisha (Allaah amridhie):

"وَلَا اعْتِكَافَ إِلَّا فِيْ مَسْجِدِ جَمَاعَةٍ"

"Na hapana Itikafu isipokuwa katika msikiti 'unaoswaliwa' jamaa"[9].

4- Fat-hul baari (Jz. 4, Uk. 271).
5- Tafsiirul Qetubi (Jz. 2, Uk. 333) na Ibn Qudama katika Al-Mughni (Jz. 3, Uk. 187).
6- Surat Al-Baqara/187.
7- Ameitaja Abdullaahi Bin Ahmad katika kitabu Al-Masaali (Jz. 2, Uk. 673). Kwa Sanadi sahihi.
8- Sahihi Sunan Abi Daud (2473).
9- Sahihi Sunan Abi Daud (2135).

Kauli ya Tano: Itikafu inakaliwa katika Masjidil Haraam (Makka) na Masjid Nnabawi (Madina), na hii ni kauli ya ‘Atwaa kama alivyoitaja Imam Abdur Razzaaq[10]:

«لَا جِوَارَ إِلَّا فِي مَسْجِدِ مَكَّةَ، وَمَسْجِدِ الْمَدِينَةِ»

“Hakuna Itikafu isipokuwa katika msikiti wa Makka na msikiti wa Madina”.

Kauli ya Sita: Itikafu inakaliwa katika msikiti wa Mtume ﷺ tu, nayo ni kauli Said Bin Musayyib (Allaah amrehemu)

«لَا اعْتِكَافَ إِلَّا فِيْ مَسْجِدِ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ»

“Hapana Itikafu isipokuwa katika msikiti wa Mtume ﷺ tu”[11].

Kauli ya Saba: Itikafu inakuwa katika misikiti mitatu tu, nayo ni kauli ya Hudhaifa (Allaah amridhie), na ametolea ushahidi kwa hadithi inayosema:

«إِنَّمَا الِاعْتِكَافُ فِي هَذِهِ الْمَسَاجِدِ الثَّلَاثَةِ: مَسْجِدِ الْحَرَامِ، وَمَسْجِدِ الْمَدِينَةِ، وَالْمَسْجِدِ الْأَقْصَى»

“Hakika Itikafu ni katika misikiti mitatu hii: Masjidil Haraam (Makka), Masjidil Nnabawi (Madina) na Masjidil Aqsa ‘Palestina’ ”[12]. Hadithi hii ndio asili ya kuandika Makala yetu hii.

Kauli yenye nguvu ni kwamba Itikafu inakaliwa katika msikiti unaoswaliwa swala za jamaa, na hii ni kauli ya Ibn Masoud, Hasanil Basri, ‘Urwa, Az-Zuhri, Is-haaq, Ibn Hazmi Ibn Taymiyyah, Imam Shaukani, Bukhari Ibn Hajar na wengine wengi.

2. DALILI ZENYE KUELEZEA ITIKAFU

Kauli ya Allaah Ta’alaa:

﴿وَلَا تُبَٰشِرُوهُنَّ وَأَنتُمۡ عَٰكِفُونَ فِي ٱلۡمَسَٰجِدِۗ﴾

“Wala msichanganyike nao (kwa jimai) na hali mnakaa Itikafu misikitini”[13].

Na imepokewa hadithi kutoka kwa Aisha (Allaah amridhie):

«أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، كَانَ يَعْتَكِفُ العَشْرَ الأَوَاخِرَ مِنْ رَمَضَانَ حَتَّى تَوَفَّاهُ اللَّهُ، ثُمَّ اعْتَكَفَ أَزْوَاجُهُ مِنْ بَعْدِهِ»

“Kwamba Mtume ﷺ, alikuwa anakaa Itikafu masiku kumi ya mwisho ya ramadhani, mpaka Allaah alipomfisha, kisha wakakaa Itikafu wakeze baada yake” **Bukhari (2026) na Muslim (1172).**

10- Al-Muswannaf (Jz. 4, Uk. 348) namba (818).
11- Al-Muswannaf (Jz. 4, Uk. 346) namba (808).
12- Al-Muswannaf (Jz. 4, Uk. 347) namba (814).
13- Surat Al-Baqara/187.

3. ITIKAFU INAKALIWA KATIKA MSIKITI UNAOSWALIWA SWALA ZA JAMAA

Amesema Imam Bukhari (Allaah amrehemu):

"بَابُ الِاعْتِكَافِ فِي العَشْرِ الأَوَاخِرِ، وَالِاعْتِكَافِ فِي المَسَاجِدِ كُلِّهَا"

“Huu ni mlango wa kukaa Itikafu katika masiku kumi ya mwisho, na kukaa Itikafu katika misikiti yote”[14].

Amesema Ibn Hazmi (Allaah amrehemu):

"وَالِاعْتِكَافُ جَائِزٌ فِي كُلِّ مَسْجِدٍ جُمِعَتْ فِيهِ الْجُمُعَةُ أَوْ لَمْ تُجْمَعْ"

“Na inafaa kukaa Itikafu katika msikiti wowote ambao huswaliwa humo Ijumaa au hapana”[15].

Amesema Ibn Qudama (Allaah amrehemu):

"وَإِنْ كَانَ اعْتِكَافُهُ مُدَّةً غَيْرَ وَقْتِ الصَّلَاةِ؛ كَلَيْلَةٍ أَوْ بَعْضِ يَوْمٍ، جَازَ فِي كُلِّ مَسْجِدٍ؛ لِعَدَمِ الْمَانِعِ..."

“Ikiwa mtu kukaa kwake Itikafu ni katika muda usiokuwa wakati wa swala, kama vile usiku au sehemu ndogo ya mchana, itafaa kukaa Itikafu katika msikiti wowote, kwa kukosekana chenye kuzuia hilo”[16].

Amesema Sheikh Fauzan (Allaah amhifadhi):

"فَلَا يَعْتَكِفُ الإِنْسَانُ فِيْ بَيْتِهِ أَوْ فِي أَيِّ مُصَلًّى يَنْفَرِدُ فِيْهِ أَوْ فِيْ مَسْجِدٍ مَهْجُوْرٍ لَا يُصَلَّى فِيْهِ ... هَذَا لَا يُعْتَكَفُ فِيْهِ وَإِنْ كَانَ فِي الأَصْلِ مَسْجِدًا؛ لِأَنَّهُ يُشْتَرَطُ فِي الِاعْتِكَافِ أَنْ يَكُوْنَ فِيْ مَسْجِدٍ تُقَامُ فِيْهِ الْجَمَاعَةِ لِأَجْلِ أَنْ يَجْمَعَ بَيْنَ الِاعْتِكَافِ وَالصَّلَاةِ مَعَ الْجَمَاعَةِ"

“Mtu asikae Itikafu nyumbani kwake wala sehemu yoyote ya kuswalia ambayo atapwekeka, wala katika msikiti uliohamwa ambao hauswaliwi ndani yake, msikiti huo haukaliwi ndani yake Itikafu ijapokuwa asili yake ni msikiti, kwa sababu inashurutiwa katika kukaa Itikafu iwe katika msikiti ambao unaswaliwa ndani yake swala za jamaa, ili akusanye baina ya Itikafu na kuswali pamoja na jamaa”[17].

Amesema Ibn Qudama (Allaah amrehemu):

"وَإِنَّمَا اشْتُرِطَ ذَلِكَ؛ لِأَنَّ الْجَمَاعَةَ وَاجِبَةٌ، وَاعْتِكَافُ الرَّجُلِ فِي مَسْجِدٍ لَا تُقَامُ فِيهِ الْجَمَاعَةُ يُفْضِي إلَى أَحَدِ أَمْرَيْنِ: إمَّا تَرْكُ الْجَمَاعَةِ الْوَاجِبَةِ، وَإِمَّا خُرُوجُهُ إلَيْهَا، فَيَتَكَرَّرُ ذَلِكَ مِنْهُ كَثِيرًا مَعَ إمْكَانِ التَّحَرُّزِ مِنْهُ، وَذَلِكَ مُنَافٍ لِلِاعْتِكَافِ،

14- Bukhari (Jz. 3, Uk. 47).
15- Al-Mughni (Jz. 2, Uk. 190).
16- Al-Muhallaa (Jz. 3, Uk. 428. [Ma-ala namba 633].
17- Al-Muntaqaa min Fataawal Fauzaan (Jz. 5, Uk. 46).

"Na hakika limeshurutishwa jambo hilo, kwa sababu (kuswali) jamaa (kwa mwanaume) ni wajibu, na mtu kukaa Itikafu katika msikiti ambao hauswaliwi swala za jamaa inapelekea kwenye moja ya mambo mawili: Kuacha swala ya jamaa ambayo ni wajibu kwake, au kutoka kuifuata hiyo jamaa, na mwisho wake litajikariri jambo hilo kwake pamoja na kuwezekana kuliepuka, na hilo linapingana na Itikafu"[18].

4. JE INAFAA KUKAA ITIKAFU KATIKA ISIYOKUWA MISIKITI MITATU 'MASJIDIL HARAAM (MAKKA), MASJIDI NNABAWI (MADINA) NA MASJIDIL AQWA (PALESTINA)?

Suala hili lina khilafu baina ya Maulamaa, pamoja kundi kubwa kati yao wanaona kufaa kukaa Itikafu katika isiyokuwa misikiti hiyo mitatu, na khilafu hiyo ni kutokana na hadithi ya Hudaifa (Allaah amridhie) inayosema:

"لَا اعْتِكَافَ إِلَّا فِيْ الْمَسَاجِدِ الثَّلَاثَةِ"

"Hapana Itikafu isipokuwa katika misikiti mitatu"[19].

Kwamba je makusudio ni hakuna kukaa Itikafu msikiti wowote zaidi ya hiyo mitatu au inafaa kukaa katika misikiti mingine lakini hapo alikuwa anakusudia kutaja misikiti iliyo bora kukaliwa Itikafu kutokana na fadhila za misikiti hiyo?

Amesema Sheikh Ibn Baaz (Allaah amrehemu):

"يَصِحُّ الِاعْتِكَافُ فِيْ غَيْرِالْمَسَاجِدِ الثَّلَاثَةِ إِلَّا أَنَّهُ يُشْتَرَطُ فِيْ الْمَسْجِدِ الَّذِيْ يُعْتَكَفُ فِيْهِ إِقَامَةُ صَلَاةِ الْجَمَاعَةِ فِيْهِ فَإِنْ كَانَتْ لَا تُقَامُ فِيْهِ صَلَاةُ الْجَمَاعَةِ لَمْ يَصِحَّ الِاعْتِكَافُ فِيْهِ"

"Inafaa kukaa Itikafu katika isiyokuwa misikiti mitatu, isipokuwa inashurutishwa uwe ni msikiti ambao zinaswaliwa ndani yake swala za jamaa, na kama haziswaliwi ndani yake swala za jamaa hafai kukaa Itikafu ndani yake"[20].

18- Al-Mughni (Jz. 3, Uk. 189).
19- As Sahiha (2786).
20- Majmuu fataawa Ibn Baaz (Jz. 15, Uk. 444).

Kadhaalika aliulizwa Sheikh Ibn Uthaimiin (Allaah amrehemu):

"هَلْ يَجُوْزُ الِاعْتِكَافُ فِيْ غَيْرِ الْمَسَاجِدِ الثَّلَاثَةِ؟"

"Je inafaa kukaa Itikafu katika isiyokuwa misikiti mitatu?"

Akajibu:

"يَجُوْزُ الِاعْتِكَافُ فِيْ غَيْرِ الْمَسَاجِدِ الثَّلَاثَةِ... وَلَوْ قُلْنَا: إِنَّ الْمُرَادَ بِهَا الْمَسَاجِدُ الثَّلَاثَةُ لَكَانَ أَكْثَرُ الْمُسْلِمِيْنَ لَا يُخَاطَبُوْنَ بِهَذِهِ الْآيَةِ، لِأَنَّ أَكْثَرَ الْمُسْلِمِيْنَ خَارِجَ مَكَّةَ وَالْمَدِيْنَةِ وَالْقُدْسِ، وَعَلَى هَذَا فَنَقُوْلُ: إِنَّ الِاعْتِكَافَ جَائِزٌ فِيْ جَمِيْعِ الْمَسَاجِدِ، وَإِذَا صَحَّ الْحَدِيْثُ... فَإِنَّ الْمُرَادَ الِاعْتِكَافُ الْأَكْمَلُ وَالْأَفْضَلُ، وَلَا شَكَّ أَنَّ الِاعْتِكَافَ فِي الْمَسَاجِدِ الثَّلَاثَةِ أَفْضَلُ مِنْ غَيْرِهِ، كَمَا أَنَّ الصَّلَاةَ فِي الْمَسَاجِدِ الثَّلَاثَةِ أَفْضَلُ مِنْ غَيْرِهَا"

"Inafaa kukaa Itikafu katika isiyokuwa misikiti mitatu... Na lau tukisema: makusudio ya (Aya) hii[21] ni misikiti mitatu tu 'basi' ingelikuwa waislamu wengi hawasemeshwi 'haiwahusu' Aya hii, kwa sababu waislamu wengi wapo nje ya Makka, Madina na Quds 'Palestina', na juu ya msingi huu tunasema: Inajuzu kukaa Itikafu katika misikiti yote, na endapo itasihi hadithi hiyo: 'kwamba Itikafu ni misikiti mitatu tu' basi inakusudiwa Itikafu iliyokamilika na iliyo bora, na hapana shaka yoyote kwamba kukaa Itikafu katika misikiti hii mitatu ni bora kuliko 'sehemu' nyingine, kama ilivyokuwa kuswali katika misikiti hiyo mitatu ni bora kuliko misikiti mingine"[(22)].

Nataraji kwa maelezo haya nimejibu swali la muulizaji na kuondoa utata uliopo katika hadithi hiyo. Ikiwa nimepatia basi ni kwa taufiq kutoka kwa Allaah na pale nilipokosea ni kwa uchache wangu wa maarifa na mapungufu ya kibinadamu.

Tunamuomba Allaah aturuzuku Ikhlaas katika maneno na vitendo.

Abu Halima Arafat,

15/ramadhani/1443h – 15/4/2022m,

Simu: 0715263253.

[21]- Alikuwa anaelezea Aya: **"Wala msichanganyike nao (kwa jimai) na hali mnakaa Itikafu misikitini"**

[22]- Majmuul fataawa warasaail Ibn Uthaymin (Jz. 20, Uk. 160).